# Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) Kwa Tanzania: Uanishaji Mpya wa Majukumu

## *Taarifa ya Kisera # 2*

**March. 2021**

## Mapendekezo ya Kisera

- Kugatua majukumu ya utelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)/Ainisha idara katika serikali za mitaa
- Kuandaa takwimu za msingi na viashiria vya kufuatilia utekelezaji, ngazi ya serikali za mitaa, kwa kushirikiana na Idara ya Takwimu (NBS)
- Kukuza uelewa wa SDGs katika jamii na hasa kwa wanawake na watu wa kawaida mitaani.
- Kuendesha kampeni za uhamasishaji wa SDGs na kujenga uwezo wa watumishi wapya na waliokuwepo, katika ngazi ya serikali za mitaa. Kampeni hizi zinaweza kujumuisha taasisi za kiraia, wasomi, wabunge n.k.
- Kufuatilia na kujifunza kutokana na uzoefu na mifano mizuri ya kisera ya kimataifa kuhusu utekelezaji wa SDGs, ikijuisha: ugatuzi wa majukumu kufikia ngazi za mitaa; na ushiriki katika programu za kuelimishana na matukio ya kimataifa na kikanda.
- Kuandaa mfumo wa kitaifa wa muda mrefu unaowiana na ajenda 2030, kusaidia mkakati wa taifa wa utelezaji wa maendeleo endelevu, chini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.
- Makampuni yajumuishe utekelezaji wa SDGs katika mifumo yao ya ripoti.
- Kuanzisha dirisha la SDGs la kufuatilia utelezaji, na kuandaa ripoti mbadala ili kujiridhisha na ripoti za serikali. Hii itasidia kuchochea mijadala mizuri ya kisiasa.
- Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano (FYDP III) ujikite zaidi katika utekelezaji wa SDG 1, 13, 14, 15 17.

## MAMBO MAKUU YALIYOIBULIWA

- Mfumo wa sasa wa uratibu, utekelezaji na tathmini kwa Tanzania ni mfumo wa kutoka juu kwenda chini badala ya mfumo wa kutoka chini kwenda juu uliopendekezwa katika Ajenda 2030 ya maendeleo endelevu.
- Kiwango cha uelewa wa SDGs ni kidogo, watu vijijini wakiwa na uelewa mdogo zaidi. Aidha, uchambuzi wa hali halisi unaonesha kwamba, kiwango cha elimu na hata jinsia, vinachangia uungwaji mkono wa SDGs.
- Wadau wengine wa ndani kama vile asasi za kiraia na sekta binafsi hawahusiki moja kwa moja na SDGs hapa Tanzania.
- Utekelezaji wa SDGs umejumuishwa katika FYDP wakati SDGs zina upeo wa muda mrefu zaidi, kufikia mwaka 2030.
- Tanzania inafanya vizuri katika malengo nane (2, 3, 4, 5, 6, 8, 10, 16). Tukiongeza juhudi, kwa kushurikiana na wadau wengine wa ndani na nje, malengo manne (7, 9,11, 12) yanaweza kufikiwa ifikapo mwaka 2030. Malengo matano (1, 13, 14, 15 17) yatahitaji nguvu ya ziada kuyafikia.




Tampere University

Pilot4DEV

IMED

COWI

PILOT4 RESEARCH AND DIALOGUE

## Utangulizi

Mwezi Septemba, 2015, Tanzania iliridhia malengo 17 ya maendeleo endelevu (SDGs), yaliyotolewa na Umoja wa Mataifa (UN), kuchochea mbio za kufikia maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2030. Wadau wengi Tanzania wanakubaliana kuhusu uharaka wa kuchukua hatua katika nyanja za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, na hifadhi ya mazingira, yanayokwaza maendeleo endelevu. Hata hivyo utayari wa kuyapokea na kukubali malengo haya kisiasa ni mdogo. Pamoja na juhudi kubwa ya Serikali na wadau wengine, ya kuridhia SDGs, juhudi hizi hazijasambaa ngazi za chini, na kuna ushirikishwaji mdogo wa wadau muhimu katika halmashauri na hata watu wa kawaida mitaani na vijijini.

Utaratibu wa maendeleo endelevu kuanzia chini kwenda juu, unaoweka mkazo na kutambua nafasi muhimu ya serikali za mitaa, asasi za kiraia, sekta binafsi na jamii kwa ujumla, unatambulika na kukubalika na wadau wa maendeleo kama vile Jumuiya ya Ulaya -EU[1].

Taarifa hii fupi imeandaliwa kwa kuzingatia mtazamo huu, na mambo yaliyojitokeza katika utafiti. Inaangazia pengo kubwa katika mfumo wa sasa wa utekelezaji wa SDGs, ambalo linapaswa kuzingatiwa na wadau wakuu. Taarifa inapendekeza utaratibu mwafaka unaoweza kufuatwa hapa Tanzania, ili kupata mafanikio makubwa zaidi katika utekelezaji wa SDGs.

Uchambuzi huu umefanyika kwa kufanya mapitio ya maandiko ya wasomi na taasisi mbalimbali, pamoja na majadiliano na watu muhimu waliowakilisha Idara Kuu ya Taifa ya Takwimu (NBS), Serikali kuu, na za mitaa, wanaohusika katika utekelezaji mikakati ya SDGs hapa Tanzania.  Vilevile Makala haya yametumia matokeo ya utafiti uliofanyika Shinyanga, Mwanza, Dodoma na Moshi uliokuwa unapima kiwango cha uelewa wa SDGs, kwa watu wa kawaida mitaani.

## Muhtasari wa Mambo Makuu Yaliyoibuliwa

### Ushirikishwaji za Serikali za Mitaa (LGAs)

Kwa sasa uratibu, utekelezaji na ufuatiliaji wa  SDGs unafanywa na Serikali kuu kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo ndiyo kituo kikuu cha mawasiliano kuhusu SDGs. Aidha Ofisi ya Waziri Mkuu ina jukumu la usimamizi ikisaidiwa na Kamati Elekezi inayojumuisha makatibu wakuu wa wizara kuu.

Katika ngazi ya halmashauri, wabunge wana nafasi ya pekee ya kuelezea ujumbe mkuu wa SDGs katika halmashauri. Aidha wabunge wana wajibu wa kuchambua bajeti ya Serikali ili kuhakikisha SDGs zimepewa kipaumbele katika matumizi ya Serikali, na zinajitokeza vizuri katika mipango na miradi ya maendeleo ya halmashauri.

Kwa mujibu wa Ajenda 2030, utekelezaji mzuri wa SDGs unatakiwa kufuata mfumo wa kutoka chini kwenda juu, kupitia serikali za mitaa, badala ya ule wa kutoka juu kwenda chini. Mpaka sasa kumekuwepo na ushirkishwaji mdogo sana wa serikali za mitaa. Maafisa wengi waliohojiwa katika ngazi ya serikali za mitaa hawakuwa na uelewa wa SDGs, na walikiri kwamba wanatekeleza tu maagizo kutoka Serikali Kuu.

***Mapendekezo Muhimu ya Kisera:***

- Kugatua jukumu la utekelezaji wa SDGs kwenda ngazi ya Halmashauri, kwa kuanisha idara maalumu (kama vile idara ya mipango) na kuipa jukumu la kuratibu SDGs katika ngazi ya serikali za mitaa.
- Kushirikiana na NBS kuandaa takwimu za msingi na viashiria vya kufuatilia utekelezaji wa SDGs katika ngazi ya serikali za mitaa.
- Kuelezea SDGs kwa jamii, na kubuni programu za kujenga uwezo katika ngazi ya halmashauri, kwa watumishi wapya na waliokuwepo. Zoezi hili lijumuishe asasi za kiraia, wasomi, wabunge nk.
- Kufuatilia na kujifunza kutokana na mifano mizuri ya kisera ya kimataifa, katika utekelezaji wa SDGs, katika ngazi za chini ya serikali kuu, na kushiriki katika programu za kuelimishana, na katika matukio mbalimbali ya kimataifa na kikanda.
- Kuongeza ushirikiano wa kisera baina ya Serikali Kuu, TAMISEMI na Wabunge ili kupata utashi wa kisiasa kwa shughuli za uhamasishaji, na pia kupata rasilimali za ndani, kwa utekelezaji mzuri wa SDGs.
- Kushirikiana na wadau wa maendeleo ili kupata utaalamu na fedha za kutosha, kwa utekelezaji wa SDGs katika ngazi za chini.

### Ushirikishwaji wa Jamii

Kukuza uelewa wa jamii kuhusu SDGs ni muhimu sana kwa utekelezaji mzuri. Kuelewa jamii inachukuliaje suala hili ni hatua ya kwanza ya ushirikishwaji wa jamii katika

[1] *Inajumuisha: Malengo ya Maendeleo Endelevu: Mambo Serikali za Mitaa Zinapswa Kuyafahamu (2015); Mpango Mahalia wa SDGs: utekelezaji na ufuatiliaji katika Ngazi za chini Kitaifa (2016).*

uhamasishaji wa SDGs. Lakini utafiti umeonesha kwamba kulikuwa na uelewa mdogo sana wa jambo hili katika ngazi za chini kitaifa. Ili kuelewa zaidi, tulifanya uchambuzi ya mtazamo wa jamii kuhusu SDGs katika mikoa minne. Uchambuzi ulionesha kuwa, asilimia 80 ya wakazi wa mijini hawatambui SDGs, na asilimia 88 ya wakazi wa vijijini hawajawahi kusikia SDGs. Aidha, utafiti unaonesha kwamba kiwango cha elimu, jinsia na mtizamo wa jamii vinachangia sana uungwaji mkono wa SDGs. Hii inamaanisha kuwa mwanaume waliohojiwa na watu waliokuwa na kiwango cha juu cha elimu walionesha kuunga mkono zaidi SDGs.

Vilevile jamii inachukulia SDGs kama jambo linalohusiana na hifadhi ya mazingira, badala ya kuhusisha na uchumi na maendeleo ya jamii. Cha kupendeza ni kwamba watu wana uelewa zaidi wa malengo ya maendeleo ya milenia (MDGs) kuliko SDGs, ikimaanisha kulikuwa na uhamasishaji zaidi wa MDGs.

***Mapendekezo Makuu ya Kisera:***

- Ili mkakati wa uhamasishaji wa SDGs upate matokeo mazuri zaidi, unapaswa kulenga makundi Fulani, badala ya kuwa na uhamashaji wa jumla tu.
- Kuhamasisha jamii yote na hasa kuwalenga wanawake na watu wa elimu ya chini.

## Ushiriki wa Wadau

Serikali inatumia wadau mbalimbali kujenga uelewa. Kuna haja ya kuanisha majukumu ya wadau mbalimbali katika utekelezaji wa SDGs. Hata hivyo, utafiti unaonesha kwamba sekta binafsi na asasi za kiraia hawahusishwi moja kwa moja katika ajenda ya SDGs. Kukubalika kwa SDGs sehemu mahalia kunategemea sana ushirikishwaji wa wadau wake, ili waone wana mchango, na hivyo kuchukulia SDGs kama mwogozo wa sera zao. Hii inamaanisha kwamba ni muhimu kushirikisha wadau moja kwa moja katika utekelezaji, tathmini na ufuatiliaji wa SDGs.

***Mapendekezo ya kisera:***

- Makampuni yanapaswa kujumuisha SDGs katika utaratibu wao wa kutoa ripoti.
- Kuanzisha dirisha la SDGs la kufuatilia utekelezaji na kuandaa ripoti mbadala, ili kujiridhisha na ukweli wa ripoti za serikali. Hii itasaidia kuchochea mijadala mizuri ya kisiasa kwa kuzingatia tofauti zitakazojitokeza katika ripoti za serikali na za wadau wengine.

## Mipango Elekezi ya Muda Mrefu

Malengo ya maendeleo endelevu -SDGs yanatekelezwa kupitia mfumo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya miaka mitano -FYDP II. Kwa hiyo utekelezaji wa mikakati ya maendeleo unalenga kufanikisha malengo ya maendeleo ya kitaifa na SDGs, na yana shabaha maalumu kwa kipindi chote cha utekelezaji. Hata hivyo kuna umuhimu wa kuwianisha mipango elekezi ya muda mrefu, yenye upeo wa zaidi ya miaka mitano, na mikakati ya kitaifa. Uchambuzi zaidi unaonesha kwamba mikakakati ya sasa haijawianishwa vizuri na Ajenda 2030 na kwa hiyo utekelezaji wake unakuwa kama kitu cha pembeni tu.

***Mapendekezo Makuu ya Kisera:***

- Kuandaa mpango elekezi wa kitaifa, wa muda mrefu, maalumu kwa Ajenda 2030, utakaoenda sambamba na mkakati wa kitaifa wa maendeleo endelevu, chini ya FYDP.

## Mapungufu Mengine Makubwa Katika Mfumo wa Tathmini ya Utelezaji wa SDGs

Kwa mujibu wa ripoti ya mapitio ya SDGs -National Review Report (VNR) (2019)[2], Tanzania inafanya vizuri katika malengo nane, SDG 2, 3, 4, 5, 6, 8, 10, 16. Tukiweza kuendeleza ushirikiano na wadau wa ndani, na kupata msaada wa kimataifa, malengo mane, SDG 7, 9, 11, 12 yanaweza kufikiwa katika muda uliowekwa, yaani mwaka 2030. Lakini malengo matano, SDG 1, 13, 14, 15, 17 yanahitaji nguvu ya ziada kufikiwa.

Katika mchakato wa kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa SDGs, haikuwezekana kupata takwamu kwa viashiria vyote vya SDGs. Ukosefu wa takwimu za msingi (baseline data) na ufinyu wa takwimu kwa baadhi ya viashiria umekwaza ufuatiliaji wa maendeleo ya utekelezaji (mfano SDG 8, SDG 13, na SDG 16) na kwa hiyo kuleta changamoto kubwa katika jitihada za kutathmini utekelezaji, kwani watafiti walilazimika kutumia viashiria na takwimu za zamani.

Madodoso yanayotumika sasa kukusanya takwimu hayakusanyi takwimu zote zitakazohitajika ili kuweza kujua mafanikio ya utekelezaji wa malengo yote kwa mujibu wa viashiria vinavyotumika. Aidha, ni vigumu kufanya uchambuzi wa kina kutokana na ukosefu wa taarifa muhimu, uhaba wa rasilimali na uwezo mdogo

[2] *2019, Wizara ya Fedha na Mipango iliandaa ripoti ya "Voluntary National Review" (VNR) kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa SDGs Tanzania, na kuiwasilisha Umoja wa Mataifa - High-Level Political Forum (HLPF), United Nations (UN).*

(katika taasisi za serikali) wa kukusanya taarifa mbadala kwa viashiria ambavyo taarifa zake hazipo.

***Mapendekezo muhimu ya kisera:***

- NBS ibuni viashiria maalumu vilivyoandaliwa mahsusi kwa ajili ya kupima utelezaji wa SDGs
- SDG 1, 13, 14, 15 17 ziingie katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano - FYDP III.

## Majumuisho: Utashi wa Kisiasa ni Muhimu

Kutokana na majadiliano hapo juu, ni wazi kwamba bado kuna pengo kati ya matarajio ya Ajenda 2030 na hali ilivyo kwa sasa. Jitihada za wadau wakuu hazitakuwa na matokeo makubwa, hasa katika sera za kitaifa, kama utashi wa kisiasa utakuwa mdogo. Madadiliano kuhusu SDGs yanapaswa kupanuliwa nje ya mazungumzo ya kisekta na kuwa na wigo mpana unaolenga jamii kwa ujumla. Dhamira thabiti ya kisiasa itaipa moyo Serikali kupanga bajeti ya kuwezesha wadau, nje ya Serikali, kushiriki kikamilifu

Taarifa hii inatilia mkazo uhuishaji wa SDGs katika jamii kwa kushirikisha serikali za mikoa, halmashauri na wadau wengine katika ngazi za chini, ili wote tushiriki na kutoa mchango wa kufanikisha malengo ya SDGs.

**Taarifa hii imeandaliwa kama sehemu ya mradi wa utafiti ujulikanao kama *“Macroeconomic and Fiscal Reforms in Tanzania amid the Implementation of the FYDP II: Positive Developments”***

Hii ni Makala ya “*Pilot4Dialogue*” ya kuchochea mjadala kuhusu resilimali za kiuchumi, sera na usimamizi wa fedha Tanzania, na kuweka uwanja mpana wa majadiliano endelevu yakijumuisha jamii na wadau binafsi kutoka mikoa tofauti.

**Kwa taarifa zaidi kuhusu mradi, tembelea tovuti www.pilot4dialogue.com au wasiliana na Bram De Smet barua pepe bram.desmet@tuni.fi**

Tampere University Pilot4DEV IMED COWI